

**OFISI YA RAISI**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA**

**SHULE YA SEKONDARI YA KADOTO,**  
S.L.P 344,  
MASWA- SIMIYU.

Tarehe .....

**Kumb.No KDTSS/J/VIL 3/01/2021**

Jina la Mwanafunzi.....

**1. MAEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE**

Ninayo furaha kubwa kukujulishwa kuwa umechaguliwa kujiunga kuanza kidato cha kwanza katika shule ya sekondari kadoto kwa mwaka 2021, ni mategemeo yangu kuwa utaitumia nafasi hii vizuri katika kuendeleza kipaji chako kwa muda wote utakaokuwa hapa shuleni. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 siku ya juma tatu na unatakiwa kuwepo shuleni tarehe hiyo. Toa taarifa mapema kama hutoripoti siku hiyo kabla hatua kali za kisheria hazijachukuliwa, mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021

**2. UTARATIBU NA HALI YA SHULE KIUJUMLA**

Shule hii ni mchanganyiko (wavulana na wasichana) wanafunzi wote wanapaswa kuwa makini kwa kuzingatia na kufuata taratibu zote za shule. Kupuuza na kukiuka taratibu za shule kwa makusudi kutasababisha mwanafunzi kuachishwa masomo. Sheria za shule zimeambatanishwa kwenye fomu hii hivyo zisome kwa umakini mkubwa na kuzielewa.

**3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

Sare za shule na vifaa ambavyo mzazi/mlezi anatakiwa kumwandalia mwanafunzi

**( a ) Sare ya shule**

- i) **Wavulana** –Suruali jozi mbili kitambaa cha damu ya mzee kiwe ni kitambaa cha suti na iwe na upana chini wa inchi kumi na sita (16) mzunguko pia suruali iwe na rinda mbili (2) kila upande na mifuko mitatu (3) mbele miwili na nyuma mmoja. Shati nyeupe mikono mifupi jozi mbili (2) , viatu vyeusi vya kufunika vyenye visigino vifupi na vyenye kufunga na kamba , na soksi nyeupe jozi mbili.
- ii) **Wasichana** – Sketi jozi mbili kitambaa cha damu ya mzee kiwe ni kitambaa cha suti mshono wa rinda box urefu wa kutosha hadi chini, mkanda wake usizidi nchi mbili (waist band), viatu vyeusi vya kufunika vyenye kisigino vifupi na vyenye kufunga na kamba na soksi nyeupe na ndefu jozi mbili, vyote vitakaguliwa hapa shuleni.
- iii) **Rangi ya Hijabu** –rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule kwa wasichana tu.

**b) Sare ya michezo**

- i) T-shirt rangi ya njano yenye nembo ya shule kwa wote (wavulana na wasichana).
- ii) Viatu vya raba kwa wote wavulana na wasichana
- iii) Traki suti ya rangi ya bluu kwa wasinana na wavulana bukta rangi ya bluu.

**4. VIFAA VYA MASOMO**

Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo siku ya kuripoti shuleni na vifaa hivyo vitakaguliwa

- i) Madaftari makubwa kumi na tano (15)
- ii) Mkebe wa vifaa vya hisabati
- iii) Dictionary ili imsaidie mwanafunzi kujifunza kiingereza kwa urahisi (ni ya lazima)
- iv) mfuko wa kubebea daftari zake. (School bag).

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.
2. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
3. Mahudhurio mazuri katika vipindi vya ndani na nje ya darasa ni muhimu.
4. Mwanafunzi haruhusiwi kuvuta sigara, kufuga kucha ndefu, kufuga ndevu kuvaa mavazi yasio na heshima, kupaka rangi ya kucha au midomo, kunyoa kipara wala kupigana au kugombana, kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
5. Kuvaa sare ya Shule wakati wote wa masomo darasani, kutoka nje ya shule ni kwa shughuli maalumu tu kama kwenda hospitalini na sio vinginevyo.

### MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZA

1. Wizi
  2. Uasherati
  3. Ubakaji
  4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungu, kubel n.k
  5. Kupigana au kupigana au kupiga
  6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
  7. Kudharau bendera ya Taifa
  8. Kuoia au kuolewa
  9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
  10. Kutoa mimba
  11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
  12. Kukataa adhabu kwa makusudi
  13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
- Naambatanisha na fomu zifuatazo
- i) Medical examination Form ambayo itatakiwa kujazwa na Mganga Mkuu wa Hospital ya Serikali. pia form hii aje nayo mwanafunzi siku ya kuripoti shuleni
  - ii) Naambatanisha pia form ya historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai
  - iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo yanayotolewa shuleni.
  - iv) Siku ya kuripoti mwanafunzi aje shuleni na Mzazi au mlezi
  - v) Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII



GREGORY C MGUMBA

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE  
SHULE YA SEKONDARI KADOT,  
S.L.P. 344 MASWA